Atasogezwa muumini siku ya Kiyama karibu na Mola wake Mlezi Aliyetakasika na Kutukuka, kisha atamuwekea pazia lake, hapo atamuonyesha wazi madhambi yake ili akiri

Kutoka kwa Swafwan bin Muhrizi amesema: Mtu mmoja alisema kumwambia bin Omari radhi za Allah ziwe juu yao, ulimsikia akisema nini Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuhusu kunong'ona? Akasema: nilimsikia akisema: "Atasogezwa muumini siku ya Kiyama karibu na Mola wake Mlezi Aliyetakasika na Kutukuka, kisha atamuwekea pazia lake, hapo atamuonyesha wazi madhambi yake ili akiri, kisha atasema: Je wayajua? Atasema: Ndiyo Mola wangu ninayajua, atasema: Basi hakika mimi nilikusitiri madhambi haya ulipokuwa duniani, na mimi ninakusamehe madhambi hayo leo hii, hapo atapewa faili la mema yake, na ama makafiri na wanafiki, wataitwa hadharani mbele ya kadamnasi, (kisha patasemwa) hawa ndio waliompinga Mwenyezi Mungu"

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuhusu Mwenyezi Mungu kunong'ona na mja wake muumini siku ya Kiyama, akasema: Atasogezwa muumini siku ya Kiyama karibu na Mola wake Mlezi kisha atamuwekea pazia lake la kumkinga na watu walioko katika kisimamo, hakuna atakayeona katika pazia hilo zaidi yake, hapo atamwambia: Je walijua dhambi fulani na fulani... atamtaka akiri madhambi yake yaliyokuwa kati ya mja na Mola wake Mlezi. Naye atasema: Ndiyo, ewe Mola Mlezi. Mpaka atakapofadhaika muumini na kuogopa, Mtukufu atamwambia: Mimi niliyasitiri kwako madhambi haya duniani, na mimi leo hii ninayasamehe kwa ajili yako, hapo atapewa faili la mema yake. Na ama kafiri na mnafiki wataitwa mbele ya kadamnasi: Hawa ndiyo waliomkadhibisha Mola wao Mlezi, basi tambueni kuwa laana za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya madhalimu.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/4242